

**TARGETER WINGS**  
**KUTATHMINI HATUA YA MWANAFUNZI**  
**GREDI 2 - 2021**



**SHUGHULI ZA KISWAHILI**  
**KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA,**  
**KUSOMA KWA SAUTI**

Jina .....

Jinsia: Mvulana

Msichana

Jina la shule .....

## KUSIKILIZA NA KUZUNGUMZA

Nitakusomea hadithi kisha utajibu maswali nitakayokuuliza.

Bakari Machachari aliishi na mama yake. Bakari hakuenda shule. Kila siku alimsaidia mamake kufanya kazi za nyumbani.

- a) Bakari aliishi na nani? \_\_\_\_\_
- b) Ni nani hakuenda shule? \_\_\_\_\_
- c) Taja kazi tatu za nyumbani. \_\_\_\_\_

## KUSOMA KWA SAUTI

Soma hadithi hii kwa sauti. Mwanafunzi asome maneno 40 kwa dakika moja.

Vidoro na Faiza walifunga mlango kwa kufuli. Walifululiza hadi kwenye ukingo wa mto. Walivua fulana wakitaka kuogelea. Mara wakasikia mtu akisema “si vizuri kuogelea mtoni. Mtachafua maji.” Mtu huyo alikuwa Fikirini, jirani yao. Alikuwa akivua samaki kwa ndoana. Walivaa fulana zao na wakasema hawataogelea mtoni tena. Wakamkaribia jirani yao.